



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA HANDENI

MsomiBora.com



MTIHANI WA PAMOJA MUHULA WA KWANZA KIDATO CHA TATU MEI 2025

KISWAHILI

021

MUDA: SAA 3

MAELEKEZO

- Mtihani huu una Sehemu tatu ambazo ni A, B na C yenye jumla ya maswali kumi (10).
- Jibu maswali yote kutoka sehemu A , B na maswali mawili (2) kutoka Sehemu C.
- Zingatia maelekezo ya kila sehemu

SEHEMU A (Alama 16)

1. Katika swali la i-x, chagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika mapendekezo uliyopewa. Andika jibu kwa herufi kubwa.
 - i. Kombo huimba nyimbo katika utaratibu wa kupanda na kushuka kwa sauti yake. Uimbaji humvutia kila anayemsikiliza. Je utaratibu huu kiisimu hujulikana kama?
A . Mkazo
B. Kiimbo
C. Lafudhi
D. Kitemeo
 - ii. "Walilima, wakupanda". Je hii ni aina gani ya sentensi?
A. Sahili
B. Ambatano
C. Shurutia
D. Changamano
 - iii. Jumla ya Silabi zinazounda mshororo huitwaje?
A. Vina
B. Bahari
C. Mizani
D. Muwala
 - iv. "Nimekufia mtoto mzuri". Huu ni mtindo gani wa Lugha?
A. Simo
B. Methali.
C. Msemo
D. Rejesta
 - v. "Shangazi yupo shambani kwake " kifungu cha maneno hiki cha maneno kipo katika ngeli ipi?
A. I -ZI
B. YU - A - WA
C. PA - MU - KU
D. KI - VI
 - vi. Ifuatayo ni moja ya sifa ya mhakiki wa kazi ya Fasihi.
A. Awe anamfahamu mwandishi kwa undani.
B. Awe amesoma kazi nyingi za Fasihi
C. Hapaswi kumpa mwandishi ari ya kuendelea na uandishi.
D. Awe zao la jamii iliyoandikiwa.
 - vii. Mtoto alikuwa mwizi .Neno alikuwa ni
A .T
C. Ts

- B. t D. U
- viii. Bakari alifurahi alipopata maswali yote ya kiswahili. Neno alipopata ni aina gani ya neno?
A. Nomini C. Kitenzi kikuu
B. Kielezi. D. Kishazi tegemezi kielezi.
- ix. Mama Fatuma hupenda kusimulia hadithi kuhusu vita vya majimaji. Je hizi ni aina gani za hadithi?
A. Tarihi. C. Vigano
B. Ngoma. D. Visasili
- x. Ufupishaji wa habari una misingi yake ambayo hapaswi kukiukwa. Ni upi misingi wa kazi hiyo?
A. Kuzingatia wazo kuu C. Kuzingatia Lugha yenye mvuto
B. Kuzingatia muundo wa kazi hiyo D. Kuzingatia mtindo wa kazi hiyo

MAJIBU

i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	ix	x

2. Oanisha maana za dhana mbalimbali za tungo katika orodha A na dhana za husika katika orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako Cha kujibia.

KIFUNGU A	KIFUNGU B
(i) Sehemu ya sentensi inayokaliwa na nomino au kikundi nomino	A. Kiarifu
(ii) Sehemu ya sentensi ambayo huarifu tendo linalotendeka	B. Chagizo
(iii) Sehemu ya sentensi inayokaliwa na mtenda wa jambo	C. Shamirisho
(iv) Sehemu ya sentensi inayokaliwa na kielezi au kikundi kielezi	D. Prediketa
(v) Sehemu ya sentensi inayokaliwa na kitenzi chenye O - rejeshi	E. Kiima
(vi) Sehemu ya sentensi inayokaliwa na kitenzi au kikundi kitenzi.	F. Kirai
	G. Kishazi tegemezi
	H. Kishazi huru

MAJIBU

i	ii	iii	iv	v	vi

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali yote katika Sehemu hii

3. a) Fafanua kwa ufupi maana ya kujua na kunea kwa Lugha.
b) Ukuaji na uneaji wa kiswahili umepitia vipindi vingi tofauti, Fafanua Kwa mifano mambo manne (04) yaliyosaidia kukuza na kueneza Lugha ya kiswahili kipindi cha Wajerumani.
4. i) Tunga sentensi kubainisha matumizi yafuatayo ya mofimu "KI"
a. Masharti c. Kitenzi kishirikishi
b. Kundelea Kwa tendo. d. Upatanisho wa kisarufi.
- ii) Kwa kila sentensi oneshwa kiima na kiarifu Kwa kutenga na kistari na kuandika "K" kwa kiima na "A" Kwa kiarifu.
a. Rais wa Tanzania alikuwa anahutubia wananchi.
b. Ng'ombe wangu mkubwa amekula majani yote.
c. Mtoto wangu amekunywa maji machafu.
d. Mwizi aliyeikamatwa jana ameachiwa.

5. . a) Bakari Silinde ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza ambaye alipewa zawadi ya kamusi Kwa kufanya vizuri katika somo la kiswahili,baada ya kufungua kamusi alikuta picha na michoro mbalimbali ambayo haikumfurahisha na kupendeza nayo na kuona kamusi haina maana yoyote.Wewe kama mtaalamu wa kiswahili muelimishe Bakari Silinde umuhimu wa michoro katika kamusi,Kwa hoja Tano (05).
b) Katgoria za maneno zilizo kuu huhusisha Katgoria nyingine ndogo ndogo ndani yake.Thibitisha usemi huu kwa kutaja aina nne (04) za vielezi katika lugha ya kiswahili.
6. .a) Kishazi tegemezi hutoa taarifa isiyojitosheleza na kutegemea kishazi huru Ili kukamilisha taarifa yake.Kwa mifano bainisha maumbo yanayounda kishazi tegemezi (hoja nne).
b) Sentensi sahili imeundwa Kwa njia tofauti tofauti fafana Kwa mifano miundo mitatu ya sentensi sahili.
7. .a) Andika visawe vya maneno yafuatayo kisha tunga sentensi moja kwa kila kisawe.
(i) Simu (ii) Chuchumaa (iii) Sifuri
b) Upatanisho wa kisarufi ni kigezo kimojawapo kati ya vigezo vya kuunda ngeli za nomino. Thibitisha dai hili Kwa kutunga sentensi mbili katika kila ngeli zifuatazo:
i) Ngeli ya pili (ii) Ngeli ya tatu (iii) Ngeli ya nne (iv) Ngeli ya tano.

8. . Soma kifungu cha Habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata :

Nchi ya Tanzania hufanya uchaguzi wake kila baada ya miaka mitano, uchaguzi mkuu huhusisha uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.Oktoba 2025 watanzania watakuwa katika pilika pilika za kuwapata viongozi wa kuwawakilisha katika changamoto zao.

Mtanzania aliyekuwa huru kuchagua viongozi atatakiwa kutimiza msharti yafuatayo;Awe amejiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura ,Awe na umri wa miaka 18 na kuendelea,Awe raia wa Tanzania na awe na akili timamu.

Uchaguzi utatakiwa ufanyike Kwa amani,wananchi wataweza kuelimishwa kupitia vyombo vya habari kama radio ,magazeti, runinga pamoja na majarida mbalimbali.Kwa kutumia vyombo hivyo vya habari, habari zitafika katika Sehemu zote za nchi yaani miji na vijijini.Kila mtanzania anapaswa kujua kwamba uchaguzi ni umuhimu kwakuwa hutupati viongozi bora,kundelesa demokrasia,kuleta mabadliko ya kiuchumi,kutatua migogoro mbalimbali pamoja na kuondoa ubaguzi . Watanzania tushikamane kuendelea Amani nchini.

MASWALI

- (a) Pendekeza kichwa Cha habari kifaacho Kwa habari hii.
- (b) Uchaguzi hufanyika kila baada ya miaka mingapi Tanzania?
(c) Taja sifa tatu (03) za mtu anayetakiwa kupiga kura.
(d) Unafikili Uchaguzi una umuhimu? Kama ndio au hapana Toa hoja tatu (03).

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili tu **(02)** kutoka katika Sehemu hii. Swali la kumi na Moja (11) ni la lazima.

9. .a) Mhakiki ni nani?
b) Eleza sifa nne (04) za Mhakiki Bora .
10. . Watoto ni maua mazuri Kwa wazazi wao lakini wakiachwa wafanye watakavyo wanaweza kupata madhara katika jamii. Kwa kutumia tamthilia mbili (02) ulizosoma jadili kauli hii.
11. . Usanaa wa fasihi hujitokeza katika vipengele mbalimbali muhimu.wa kutoa maana ya Sanaa, Eleza vipengele vinne (04) vinavyoonyesha usanaa wa fasihi.